Mifumo ya Chakula, Matumizi ya Ardhi na Urejeshaji katika Mandhari za Misitu ya Tanzania

# MPANGO WA USHIRIKISHAJI WA WADAU

**MRADI WA FOLUR - TANZANIA**

# MUHTASARI WA UTENDAJI

## 1. Utangulizi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Idara ya Misitu na Nyuki ya Wizara ya Maliasili na Utalii imejipatia mgao wa fedha kutoka Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) chini ya Programu ya Mifumo ya Chakula, Matumizi Ardhi na Urejeshaji (FOLUR). Ufadhili wa Mradi unapokelewa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango. Mradi upo Zanzibar na Tanzania Bara, ukilenga mandhari mbili zilizopewa kipaumbele, mandhari ya Kilombero iliyopo Tanzania Bara na Wilaya ya Kaskazini A ya Zanzibar, ukiunganisha na hatua za kitaifa za kushughulikia masuala ya kibiashara na mnyororo wa thamani katika kusaidia ukuaji wa kiuchumi wa muda mrefu wa mandhari hizi, na kwa ujumla maendeleo ya kilimo cha Tanzania.

Idara ya Misitu na Nyuki (FBD) ya Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT) itakuwa Wakala Mtekelezaji wa Kitaifa wa kutekeleza mradi kwa niaba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania (URT). Idara (FBD) itakuwa na majukumu ya kuratibu na kusimamia Washirika Watekelezaji wote wa msingi wa kitaifa, Mamlaka za Kisheria, Mamlaka za Mikoa na Wilaya, Sekta Binafsi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Asasi za Kiraia, Jamii za wenyeji.

Madhumuni makuu ya mradi ni kukuza usimamizi jumuishi wa ardhi na maji, urejeshaji, na minyororo ya thamani endelevu ya mpunga ili kuzuia ukataji miti katika mandhari zilizopewa kipaumbele Tanzania. Mradi una vipengele vinne (4), ambavyo ni:

- **Kipengele cha 1 – Kuendeleza Mifumo ya Usimamizi Jumuishi wa Mandhari:** inahusisha matumizi ya mbinu za Usimamizi Jumuishi wa Mandhari (ILM), pamoja na kuendeleza mipango ya matumizi ya ardhi na mipango inayohusiana na ulinzi wa maji, na kuifanyia kazi itekelezwe kwa kuweka mazingira wezeshi. Hapa mradi unatafuta kuimarisha maendeleo ya mbinu ya ILM kwa mandhari zilizolengwa, kwa kupitia mchakato wa wadau wengi, ili kuweka mfumo wa usimamizi wa mandhari wenye kutoa nafasi kwa uzalishaji wa mpunga.
- **Kipengele cha 2 – Kukuza mbinu za uzalishaji chakula endelevu na minyororo ya thamani inayohusika:** Kipengele kinatafuta kusaidia maendeleo ya minyororo ya thamani/usambazaji endelevu na wa kijamii wa sekta ya uzalishaji wa mpunga, pamoja na kuendeleza mbinu za kusaidia utawala, fedha na masoko ambazo zitaendesha minyororo ya thamani endelevu.
- **Kipengele cha 3 – Hifadhi na urejeshaji wa makazi ya asili:** kitahusisha kuendeleza na kutekeleza shughuli thabiti za urejeshaji wa mandhari katika mandhari zilizolengwa, pamoja na kuweka mazingira ya kuwezesha kuzisambaza.
- **Kipengele cha 4 – Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini ya Mradi:** unalenga kwenye uratibu, ushirikiano, ufuatiliaji na tathmini, pamoja na ushirikishaji wa maarifa, mafunzo, na usanisi na mawasilisho ya uzoefu Kitaifa na Kimkoa (angalia sehemu inayofuata).

## 2. Taratibu na Mahitaji

Maudhui yaliyowasilishwa hapa kwa ajili ya Mpango wa Ushirikishaji wa Wadau yameandaliwa na Mradi wa FOLUR Tanzania kwa ajili ya kuongoza ushiriki wa wadau wakati wa kuendeleza/kubuni,

kupanga, kutekeleza na kufunga mradi. Hivyo, Mpango unaweka wazi viwango, miongozo na shughuli mahsusi kwa ajili ya Mradi ili kuhakikisha uwazi, ujumuishaji, uwajibikaji, uadilifu, na ushiriki wenye ufanisi wa pande zote zitakazoathirika na mradi. Idara ya Misitu na Nyuki/Wizara ya Maliasili na Utalii ni Mpendekezaji Mkuu wa Mradi wa FOLUR wa Tanzania na ina wajibu wa kutekeleza Mpango huu wa Ushirikishaji wa Wadau. Maandalizi na utekelezaji wa Mpango wa Ushiriki wa Wadau unaongozwa na sera na miongozo ya GEF, sera za Mfuko wa Dunia wa Wanyamapori Amerika (ambaye ni Msimamizi wa Mradi wa GEF) na mahitaji ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 3. Muhtasari wa shughuli za awali za ushirikishwaji wa wadau

Mradi tayari umeshafanya baadhi ya shughuli za ushirikishaji wa wadau wakati wa hatua ya maandalizi. Shughuli hizo ni semina na mikutano ya wadau, mashauriano katika ngazi ya uwandani, mashauriano na wadau wakuu wa mradi pamoja na washiriki, kuwasilisha na kukutana na majukwaa mengine yaliyopo. Mashauriano katika ngazi ya uwandani yalihusisha mikutano na wadau wa ndani, makundi ya jamii, kutembelea maeneo, ukaguzi wa mashamba, na majadiliano ya kikundi. Mashauriano na wadau wa mradi huu yalianza hatua za awali na kuendelea na majadiliano ya kina kwa muda wa miaka miwili.

## 4. Wadau wa Mradi

Wadau ambao wametambuliwa kwa mradi huu, wamegawanyika katika makundi yafuatayo:

- **Serikali:** Hii inajumuisha Wizara, Mamlaka za Kisheria na Mawakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ngazi ya Mkoa na Wilaya pamoja na Taasisi za Utafiti ambazo aidha zina majukumu au zinavutiwa kufanya shughuli zinazohusiana na mradi. Hizi zinajumuisha Washirika wa msingi wa mradi, ambao wanawajibika kutekeleza shughuli na kufanya kazi pamoja na jamii za wenyeji katika maeneo ya mradi.

- **Jamii za Wenyeji:** Hapa ni pale ambapo Mpango wa Ushirikishaji utaangalia zaidi ukizingatia kwamba Mradi utaathiri wanajamii wote moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Jamii za wenyeji zinazotajwa hapa ni idadi ya watu ambao kwa sasa wanaishi na wana makazi ya kudumu katika maeneo ya mradi (vijiji na shehia) katika mandhari mbili za Kilombero na Unguja Kaskazini.

- **Mashirika ya Kiraia:** Hii inahusu watendaji wasio wa kiserikali wa nchini na wa kimataifa ambao wanafanya kazi katika maeneo ya mradi au ambao wana shughuli zinazohusiana na madhumuni ya mradi. Kama ilivyo kwa serikali katika upande wa jukumu linalowezekana, Mashirika ya Kiraia mengi yatakuwa washiriki wa mradi katika utekelezaji na hivyo yatajishirikisha na jamii za wenyeji katika maeneo ya mradi.

- **Sekta Binafsi na Wawekezaji wa Kifedha:** Hii inajumuisha makampuni yanayopenda kujihusisha na uwekezaji wa kibiashara na kifedha katika vipengele vinavyohusiana na madhumuni ya mradi.

- **Wanasiasa:** Hii inajumuisha Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji/Shehia katika maeneo ya mradi na katika wilaya ambazo ni wawakilishi wa jamii za wenyeji wanaoishi katika maeneo ya mradi.

Wadau hawa watajulishwa kuhusu mradi na kushirikishwa kama ilivyo kwenye mpango uliofafanuliwa zaidi katika nyaraka hii. Mchakato wa kutambua na kuonesha wajibu na majukumu ya wadau ni mchakato unaoendelea. Orodha iliyotolewa hapa itatumika kama nyaraka halisi kwa ajili ya kuchagua mazingira yanayobadilika ya kijamii, kiuchumi na kiuchumi katika mzunguko wa mradi.

## 5. Mpango wa Ushirikishaji wa Wadau

Wakala wa Utekelezaji, Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT)/Idara ya Misitu na Nyuki (FBD), inatarajia kutekeleza mradi kwa uwazi, kwa namna inayojumuisha na kwa njia inayoonesha hali halisi iliyopo. Kutokana na suala hili, mradi utatumia njia zifuatazo:

### Mkakati wa kujumuisha mtazamo wa wanawake na makundi mengine yanayohusika (walio wachache, wazee, vijana na makundi mengine yaliyotengwa)

- Mbinu mchanganyiko zitatumika wakati wa kushauriana na kushirikisha jamii, huku mitazamo na maarifa ya washiriki ikiheshimiwa, ikijumuisha: majadiliano ya kikundi kwa kutumia vigezo mbalimbali kutegemeana na hali (kwa shughuli za kiuchumi, kikundi cha umri, jinsia, eneo la kijiografia, n.k.); majadiliano na watoa taarifa muhimu msisitizo ukiwa kwa wanawake na makundi ya kuhamahama kwenye mada maalum (k.m. kuelewa mtazamo wa kihistoria wa baadhi ya shughuli, mtazamo wa makundi ya walio katika mazingira hatarishi kama vile makundi ya kuhamahama ya Wamasai na Wabarabaig ambao wanaweza wasiowepo kwenye jamii wakati wowote, mtazamo wa jinsia na hali halisi, n.k.); na mikutano ya vijiji/shehia.
- Katika kushauriana na kushirikisha wanawake, jamii za wanaohamahama na makundi mengine yaliyo katika mazingira magumu, mawasiliano yatatumika yanayolingana na muktadha wa eneo na hii itasaidia kujiamini. Katika mikutano yote, Kiswahili kitatumika na pale penye ulazima, tafsiri itatumika kwa Kiswahili na lugha za makabila kwa kutumia wanajamii. Majadiliano katika ngazi ya jamii yataongozwa na wanajamii na maafisa kutoka serikali ya wilaya.
- Rejesta itawekwa, itatengenezwa upya mara kwa mara na mifumo ya mrejesho itaundwa ili kuhakikisha kuwa wanawake na makundi mengine husika (walio wachache, wazee, vijana na makundi mengine yaliyotengwa) wanahusishwa kikamilifu katika mashauriano, wananufaika kutokana na mradi na wanataarifiwa maendeleo ya mradi.

### Mbinu zinazopendekezwa kupata mrejesho na kuhakikisha mawasiliano na wadau yanaendelea

- Wadau wote ambao wamefanya mashauriano na kutambuliwa watawekwa kwenye rejesta na itasasishwa mara kwa mara. Wadau hawa watahabarishwa vizuri taarifa za utekelezaji wa mradi na watahimizwa kutoa mrejesho na watu wanaohusika kutekeleza mradi kupitia njia mbalimbali pamoja na zikijumuisha kupigiwa simu, baruapepe, mikutano isiyo maalum miongoni mwa nyinginezo.
- Wizara za Kitaifa na Mawakala ambao ni washiriki wa msingi wa mradi watatoa mrejesho kwenye mradi kupitia mikutano (au warsha), ikijumuisha Kamati mbalimbali za Kiufundi na za Uendeshaji ambazo zimewekwa chini ya mradi, katika kubuni na kutekeleza shughuli katika mzunguko mzima wa mradi. Washiriki wa msingi pia watatoa mrejesho kupitia ushiriki wa moja kwa moja na Kitengo cha Usimamizi wa Mradi (PMU) na Vitengo vya Uratibu wa Mandhari (LCUs) viwili wakati wa kuendeleza na utekelezaji wa shughuli katika mzunguko

mzima wa mradi.

- Mpangilio wa Kitaasisi wa Mradi umetenga majukumu kwa wahusika wote kufuatilia na kukusanya mrejesho kutoka kwa jamii na wadau wengine katika mzunguko wote wa mradi. Mpangilio huu utaruhusu kukusanya, kuchambua, kufuatilia, kuwajibika na kuunganisha mrejesho uliotolewa.

- PMU, LCU, Washirika Watekelezaji na Washirika wataandika maelezo wakati wa mikutano ya vijiji/shehia, mahojiano, majadiliano ya kikundi na wakati wanatekeleza majukumu yao pamoja na jamii. Maelezo haya yatatumika kuandika na kuchambua ripoti na kuhakiki ufuatiliaji ili kutoa mrejesho kwenye utekelezaji wa mradi.

- Wanasiasa ikijumuisha viongozi wa mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa watahusishwa kutoa mrejesho kupitia hotuba wakati wa ufunguzi wa warsha, uzinduzi wa ripoti na majukwaa. Wanasiasa watashirikishwa na kufanya mashauriano ili kutoa mrejesho wao kupitia ziara kwenye ofisi za wilaya na mkoa wakati wa kuzindua shughuli za mradi. Mwenyeji wa LCU katika ngazi ya wilaya atatoa ushiriki wa siku kwa siku wa wanasiasa.

- Kama ilivyofanyika wakati wa mchakato wa kubuni mradi, wadau wengine wote (mf. Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi) ambao tayari wameshatambuliwa, wataalikwa kwenye warsha na mikutano kulingana na mada na maslahi yao ili kutoa mchango na mrejesho wakati wa kubuni shughuli, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mradi. Wadau hawa watahusishwa kupitia mashauriano ya mtu binafsi (simu, barua pepe), kushirikishana ripoti (warsha, ufuatiliaji) ambapo mrejesho unaweza kutolewa kwa PMU.

- Wizara za Kiserikali ngazi ya Taifa, Mawakala, wajumbe wa PMU na LCU pia watauwakilisha mradi katika mikutano ya wadau mbalimbali ya ndani na kimataifa, majukwaa na warsha (mf. Jukwaa la Wadau Mbalimbali la Kilombero) ambapo mrejesho unaweza kutolewa. Ushirikishaji huu utawezesha kupata mrejesho kutoka kwa wadau mbalimbali walioalikwa, na kuunda mashirikiano mapya ya wadau zaidi ya wale ambao wameshatambuliwa.

## Shughuli nyingine za ushirikishaji

- Mafunzo na kujenga uwezo kwa washirika wa mradi, watakaoathirika na wadau wenye maslahi. Mradi utajenga uwezo kwenye michakato ya wadau mbalimbali iliyopo na kuanzisha majukwaa ili kutoa nafasi ya mashirikiano na mashauriano na wadau zaidi ya wale wanaoathirika moja kwa moja na mradi.

- Utekelezaji wa mbinu za ushirikishwaji zilizooneshwa kwenye Mpango wa Ushirikishaji zinahakikisha kuwa wadau na makundi husika yanaelewa taarifa za kiufundi za mradi bila kujali kiwango chao cha elimu na

- Katika mikutano yote (binafsi, ziara za maeneo, warsha, majadiliano ya kikundi, watoa taarifa muhimu) kumbukumbu zitahifadhiwa na kuwekwa kwenye nyaraka kwa ajili ya uchambuzi na ripoti mbalimbali zitaandaliwa. Nyaraka pia zitatumika kuwafanya wadau wawe na taarifa katika ngazi mbalimbali kuhusu maendeleo, changamoto, mambo hatarishi, na fursa zinazojitokeza.

- Wilaya na jamii zitashiriki katika kubuni, kutoa maamuzi na kutoa mrejesho katika mzunguko wote wa mradi. Watendaji waliotambuliwa wa serikali na wasio wa kiserikali katika ngazi ya wilaya na jamii sio kwamba ni wanufaika tu (au pande zilizoathirika) bali pia ni washirika kwa mradi.

- Ushirikishaji wa mradi katika ngazi ya jamii utajumuisha mikutano ya Vijiji/Shehia (mikutano ya wazi), mikutano ya Kamati za Vijiji/Shehia (mf. kilimo, maliasili), majadiliano ya kikundi na watoa taarifa muhimu. Jamii itajulishwa na kushirikishwa kupitia mbinu zote za kimila (kienyeji) na za kisasa kwa kuzingatia ubora wa mitandao ya simu, hali ya hewa, na barabara zinazopitika ili kuhakikisha makundi yote yanafikiwa vya kutosha (ikijumuisha watu wenye ulemavu na wasiojua kusoma). Mbinu za kimila zitakazotumika katika kujulisha wanakijiji kuhudhuria mikutano zitajumuisha mbiu (kama inavyotumika Tanzania Bara) au upatu (kama kawaida inavyotumika Zanzibar) ambayo inahusisha matumizi ya kupiga ngoma, kugonga chuma, tarumbeta au kutembelea vitongoji, misikitini na makanisani. Njia za kisasa zitahusisha kutangaza taarifa mbalimbali za maendeleo na za mikutano itakayofanyika katika mbao za matangazo za vijiji/shehia, kutoa taarifa za mikutano kwa njia ya simu, barua, matangazo ya umma kwa kutumia vipaza sauti, kusambaza vipeperushi/barua kwa kutumia pikipiki. Taarifa za mikutano zitatolewa mapema katika ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji/Shehia.
- Katika ngazi ya jamii, viongozi wa ngazi ya vijiji/shehia watachukua majukumu mengi katika kutekeleza shughuli na hivyo watakuwa kama daraja muhimu la kuhakikisha ushiriki wa mara kwa mara na unaoendelea wa wanajamii. Viongozi wa Vijiji/Shehia utajumuisha maafisa wa serikali, na viongozi wa kuchaguliwa pamoja na kamati mbalimbali ambazo zinaunda serikali ya Kijiji/Shehia. Ushiriki katika ngazi ya jamii pia utajumuisha majukumu ya maafisa katika ngazi ya Kata, Maafisa Ugani na Maafisa Maendeleo ya Jamii.

## 6. Rasilimali na Majukumu

Wakala Mtekelezaji, MNRT/FDB, ana jukumu la ujumla na uangalizi wa kutekeleza shughuli za ushiriki wa wadau ambazo zinajumuisha mashauriano na kuarifiana. Wajibu wao ukiachia majukumu ya jumla na uangalizi, yatajumuisha kuwezesha PMU ngazi ya Taifa katika:

- Kuarifu na kutoa taarifa za utekelezaji pamoja na nyaraka nyingine muhimu kwa wakati unaofaa uliokubalika na kwa uwazi.
- Kusimamia na kutoa idhini ya utoaji wa taarifa zinazohusiana na mradi kwa njia zote za mawasiliano; na
- Kuongoza michakato ya mashauriano ngazi ya kitaifa kwa shughuli za kitaifa pamoja na washirika wa mradi

Wajibu wa kushirikisha wadau unakabidhiwa kwa washirika wote wa mradi katika kutekeleza shughuli zao, huku MNRT/FBD ikitoa wajibu wa uangalizi katika ngazi ya Taifa, na Mratibu wa Mradi/Mtaalamu wa Mifumo Endelevu ya Chakula binafsi akiwa na wajibu wa kusimamia mahusiano na wadau wa mradi, na kwa upana zaidi utekelezaji wenye ufanisi wa Mpango wa Ushirikishaji wa Wadau. Mratibu wa Mradi/Mtaalamu wa Mifumo Endelevu ya Chakula atasaidiwa, miongoni mwa wengine, na Mtaalamu wa Jinsia na Hifadhi (katika msingi wa ushauri)

Vitengo vya Uratibu wa Mandhari (LCUs), ambavyo ni sehemu ya Kitengo cha Usimamizi wa Mradi (PMU) katika ngazi ya mandhari, vitakuwa katika mstari wa mbele wa mradi na kushirikisha pande zote zitakazoathirika (moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja) kila siku. Wajibu wa LCUs ni pamoja na utekelezaji, ufuatiliaji na usimamizi wa Mpango wa Ushirikishaji wa Wadau katika ngazi ya mandhari zilizolengwa, kwa uratibu na Kitengo Kikuu cha Usimamizi wa Mradi (PMU) kilichopo MNRT/FBD. Jukumu muhimu, katika suala hili, lipo kwa Waratibu wa Programu ya Mandhari wanaohusika, wanaofanya kazi kwa kushirikiana na wafanyakazi wengine wa kiufundi.

## 7. Utaratibu wa Malalamiko

MNRT/FBD itajulisha na kushirikisha jamii kutoa mwongozo na kuhakikisha ambapo watakaoathirika na utekelezaji wa shughuli za mradi wanaweza kuwasilisha/kueleza malalamiko yao (madai au wasiwasi) na kutafuta ufumbuzi. Utaratibu wa malalamiko utakuwa rahisi, unaoeleweka na utatafuta kumlinda mlalamikaji kwa masuala nyeti. Katika hatua zote za kuripoti na kutatua malalamiko na wasiwasi, MNRT/FBD itahakikisha kuwa kuna maandishi stahiki na kwa wakati unaofaa ya hatua zote na maamuzi yaliochukuliwa. Hii itahakikisha kuwa kujiamini, haki, uwazi na mafundisho ya kuepuka hapo baadaye katika utekelezaji wa mradi.

Maelezo ya kikamilifu ya utaratibu wa malalamiko utakaoanzishwa na mradi yamewasilishwa katika Mfumo wa Athari za Mazingira na Jamii.

Kwa kuongezea kwenye utaratibu wa malalamiko ngazi ya mradi, wadau wanaweza kuwasilisha malalamiko yao kwa Wakala wa WWF GEF. Maelekezo yametolewa katika tovuti ya WWF (kama ilivyo hapo chini) pamoja na maelezo ya mawasiliano na utaratibu.

Malalamiko yote yatachunguzwa na kujibiwa ndani ya siku 10 za kazi tangu kupokelewa. Malalamiko pamoja na majibu yatawekwa kwenye kumbukumbu za ufuatiliaji wa mradi. Kama mlalamikaji hajaridhika na majibu, malalamiko yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja kwa Wakala wa Mradi GEF wa WWF US.

Lalamiko linaweza kufunguliwa na Afisa Malalamiko wa Mradi (PCO), mtumishi wa WWF ambaye yuko huru kabisa na Timu ya Mradi, mwenye jukumu la Uwajibikaji na Utaratibu wa Malalamiko wa WWF ambaye anaweza kupatikana kwa:

Baruapepe: SafeguardsComplaint@wwfus.org
Anuani ya Posta:

Project Complaints Officer
Safeguards Complaints,
World Wildlife Fund
1250 24th Street NW
Washington, DC 20037

PCO atatoa majibu ndani ya siku 10 za kazi toka kupokelewa, na malalamiko yatafunguliwa na kuwekwa kwenye ufuatiliaji wa mradi.

Wadau pia wanaweza kuwasilisha malalamiko ya kwa njia ya mtandao au kwa simu kupitia EthicsPoint, Jukwaa huru la mhusika wa tatu kwa:

*https://secure.ethicspoint.com/domain/media/en/gui/59041/index.html.*

## 8. Ufuatiliaji na Utoaji Taarifa

Wanufaika walengwa na makundi yaliyoathirika na mradi hawatakuwa chanzo tu cha taarifa bali pia watatoa uchambuzi wa hali kwa ajili ya ufuatiliaji na utoaji taarifa. Kutokana na hili, mchakato wa kufuatilia na kutoa taarifa za maendeleo ya ushiriki wa wadau utajumuisha na kuhusisha wanufaika walengwa na makundi yaliyoathirika katika mzunguko wote wa mradi.

Katika mradi mzima, yafuatayo yatahusika wakati wa ufuatiliaji:

- Shughuli zinazohusiana na ushirikishaji wa wadau zitawekwa kwenye kumbukumbu na kuripotiwa na PMU na LCUs kwa msingi wa nusu mwaka (kama sehemu ya taarifa za mara kwa mara). Ziara za ufuatiliaji na mikutano itakayofanyika zitawekwa kwenye kumbukumbu na mrejesho kuripotiwa kwa jamii (kupitia njia ambazo tayari zimetambuliwa) na wadau wenye wasiwasi au maslahi na eneo au shughuli.
- Wahusika wengine walio huru wataalikwa kuthibitisha utekelezaji wa Mpango huu wa Ushiriki wa Wadau na malengo mengine ya mradi. Hii itawezesha uwazi, itajenga kujiamini na kuhimiza maoni ya wazi.
- Wakala wa WWF GEF pia atahusika katika ufuatiliaji kwa kusudi la kusaidia mradi na kusaidia masuala yanayoathiri utekelezaji wa mradi kwa wakati muafaka na kwa ubora. Wakala wa WWF US GEF atahakiki ubora wa matokeo na maendeleo dhidi ya Mpango wa Ushirikishaji wa Wadau.
- Kamati ya Utendaji ya Mradi (PSC) pia itahusika katika kufuatilia mradi kuendana na mpango angalau mara mbili kwa mwaka na kushauri (au kuchukua ushauri) ipasavyo na kwa kiwango kilichowekwa mbele kwa ajili ya Mpango wa Ushirikishaji wa Wadau.